JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MUHTASARI WA MFUMO WA SERA ZA JUMLA ZA UCHUMI NA MAENDELEO YA JAMII KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2004/05 - 2006/07



Umetolewa na:

OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UBINAFSISHAJI
DAR ES SALAAM – TANZANIA
Aprili, 2004

Muhtasari wa Mfumo wa Sera za Jumla za Uchumi na Maendeleo ya Jamii katika Kipindi cha Mwaka 2004/05 - 2006/07

YALIYOMO

Ukurasa

Utangulizi 1
Mapitio ya Mwenendo wa Uchumi katika Mwaka 2003/04 1
Ukuaji wa Pato la Taifa 1
Kasi ya Upandaji Bei 2
Mapato na Matumizi ya Serikali 2
Deni la Taifa 3
Ujazi wa Fedha na Karadha 4
Sekta ya Nje 5
Ukuaji wa Sekta Binafsi, Uwekezaji, na Marekebisho ya Mashirika ya Umma 5
Maendeleo ya Jamii na Mkakati wa Kupunguza Umaskini 6
Masuala Muhimu ya Kisera Yaliyojitokeza Mwaka 2003/04 7
Misingi na Malengo ya Sera za Uchumi Jumla na Maendeleo ya Jamii katika Kipindi cha Muda wa Kati (2004/05 – 2006/07) 10
Misingi ya Matarajio 10
Malengo ya Sera za Uchumi Jumla na Maendeleo Ya Jamii 10
Hitimisho 11

UTANGULIZI

1. Taarifa hii inachambua mwenendo wa viashirio muhimu katika uchumi na maendeleo ya jamii katika mwaka 2003/04, inabainisha masuala muhimu ya kisera ya uchumi jumla yaliyojitokeza, na kutoa mwelekeo wa sera za jumla zitakazosukuma kasi ya ukuaji wa uchumi, kupunguza umaskini, na kuboresha maendeleo ya jamii katika miaka mitatu ijayo, 2004/05 – 2006/07. Sera za jumla za uchumi na maendeleo ya jamii zitaongoza uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Muda wa Kati na Bajeti katika kipindi cha mwaka 2004/05 – 2006/07.

MAPITIO YA MWENENDO WA UCHUMI KATIKA MWAKA 2003/04

Ukuaji wa Pato la Taifa

2. Baada ya miaka sita mfululizo ya ongezeko katika ukuaji wa Pato la Taifa, hadi kufikia asilimia 6.2 mwaka 2002, hali ya ukame iliyolikumba taifa msimu wa 2002/03, iliathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kiwango kikubwa, na hivyo kusababisha kupunguza kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 5.6 mwaka 2003. Matokeo hayo ya ukuaji ni pungufu kidogo na lengo la asilimia 5.7 lililowekwa baada ya kuzingatia hali ya ukame huo. Sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 4.0, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.0 mwaka 2002. Upungufu katika kasi ya ukuaji wa Pato la kisekta ulijitokeza katika sekta madini, biashara, mawasiliano na uchukuzi kutokana na sababu mbalimbali. Kasi ya ukuaji wa sekta ya madini ulipungua kufikia asilimia 14.3, ikilinganishwa na asilimia 15.0 mwaka 2002, kutokana na kukamilika kwa miradi mikubwa ya madini mwaka uliotangulia. Sekta ya biashara (ikijumuisha utalii) iliathirika kiasi kutokana na mashaka ya usalama/ugaidi duniani, hali ambayo imechangia kupunguza ukuaji wa sekta kuwa asilia 6.5, ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2002. Ukuaji katika sekta ya uzalishaji viwandani umeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, kadri viwanda vinavyofufuliwa baada ya ubinafsishaji na kuongezeka kwa uwekezaji mpya katika sekta hiyo. Ukuaji wa sekta hiyo ulifikia asiliamia 8.6, ikilinganishwa na asilimia 8.0 mwaka 2002. Jedwali Na. 2 na 3 katika Kiambatisho A linaonyesha mwenendo wa ukuaji wa Pato la Taifa kisekta mwaka 1999 – 2003 na matarajio kufikia mwaka 2007. Jedwali Na. 1 ni muhtasari wa mwenendo wa viashirio muhimu katika uchumi jumla.

Kasi ya Upandaji Bei

3. Mafanikio katika kutengamaza mwenendo wa uchumi nchini yanajidhihirisha katika kasi ndogo ya kasi ya upandaji bei, ambayo ilikuwa chini ya asilimia 4.5 kwa kipindi kikubwa cha mwaka 2003. Kasi ya upandaji bei katika miezi ya Februari na Machi 2003, ilikuwa asilimia 4.2, kiasi ambacho hakijawahi kufikiwa katika miongo mitatu iliyopita. Hata hivyo, hali ya ukame iliyojitokeza, ilisababisha upungufu mkubwa wa chakula kipindi cha kuelekea mwisho wa mwaka; iliyosababisha bei za vyakula kupanda, na hivyo kuongeza kasi ya upandaji bei kuanzia mwezi wa Oktoba 2003. Kasi ya upandaji bei iliendelea kupanda hadi kufikia asilimia 4.8 mwezi Machi 2004. Bei za mafuta ya petroli zilizoanza kupanda mwanzoni mwa mwaka 2004, kutokana na ongezeko la bei za mafuta ghafi katika soko la dunia, nazo zilichangia katika ongezeko hilo la kasi ya upandaji bei. Juhudi za serikali katika kufanikisha kupatikana chakula katika kipindi hicho cha upungufu imesaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti ongezeko la bei za vyakula. Mavuno yajayo yanatarajiwa kuongeza upatikanaji na usambazaji wa chakula nchini; hali itakayopunguza kasi ya upandaji huo kuelekea kwenye lengo la asilimia 4.0 ifikapo Juni 2005. Athari za kuendelea kupanda kwa bei ya mafuta katika uchumi hazijabainika kikamilifu kwa sasa, lakini inategemewa kuwa hatua za kimataifa zitachukuliwa kutengemaza bei za mafuta ghafi.

Mapato na Matumizi ya Serikali

4. Katika kipindi cha robo tatu ya mwaka wa fedha 2003/04 (Julai 2003 – Machi 2004), mapato halisi ya ndani yalifikia sh. 1,089,262 milioni, ikilinganishwa na makisio ya sh. 1,050,866 milioni, ikiwa zaidi ya makisio ya kipindi hicho kwa asilimia 3.7, kutokana na ukusanyaji mzuri wa kodi ya mapato na kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kulikochangiwa kwa kiasi kikubwa na kuongezeka kwa ufanisi katika idara husika za TRA. Katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha uliotangulia, mapato ya ndani yalifikia sh. 892,252.2 milioni. Ni dhahiri kuwa mapato ya ndani yamekuwa ya kuridhisha; na kwa mwenendo huu, kuna uwezekano mkubwa kwamba mapato yatavuka lengo la mwaka mzima wa 2003/04.

5. Jumla ya matumizi ya Serikali katika kipindi cha Julai 2003 – Machi 2004 yalifikia sh. 1,722,612 milioni, sawa na asilimia 91.2 ya makisio ya sh. 1,889,207 milioni kwa kipindi hicho. Kati ya fedha hizo, sh. 422,559 milioni zilitumika katika miradi ya maendeleo, ikiwa sawa na asilimia 72 ya makisio ya sh. 587,930 milioni kwa kipindi hicho. Matumizi ya kawaida katika kipindi hicho yalifikia sh. 1,300,053 milioni. Pamoja na kwamba kuna ongezeko katika matumizi ya Serikali ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2002/03, kutofikiwa kwa malengo kulitokana na uchanga wa uzoefu katika utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya 2001 pamoja na ucheleweshaji wa taarifa za matumizi. Kwa kutambua hayo, Serikali inafanya mapitio yenye lengo la kuboresha utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2001. Waraka wa Mfumo wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2004/05 utakaotolewa na Wizara ya Fedha, utabainisha kwa kina, mwenendo katika mapato na matumizi ya Serikali.

Deni la Taifa

6. Hadi Desemba 2003, deni la taifa (ikijumuisha la ndani na nje) lilikuwa dola za Marekani 8,755.0 milioni, sehemu kubwa ikiwa ni deni la nje (asilimia 90.1). Deni la nje liliongezeka kufikia dola 7,890.7 milioni, kutoka dola 7,268.1 milioni mwaka 2002, kutokana hasa na malimbikizo ya riba kwa madeni ambayo hayajasamehewa (non-Paris Club) na kutolewa kwa madeni mapya. Serikali imeendelea kupata misamaha ya deni la nje kutoka kwa mashirika ya kimataifa ya fedha (WB, IMF na ADB) na nchi za Paris Club. Hata hivyo, nchi nyingi nje ya kundi la Paris Club bado hazijakubali maombi ya Serikali ya kutoa nafuu ya madeni yao kwa utaratibu wa Paris Club, na hivyo majadiliano yanaendelea. Kama inavyoelekezwa katika Mkakati wa Deni la Taifa uliozinduliwa Agosti 2002, Serikali inaendelea kubadilisha madeni yake ya ndani, katika dhamana zinazouzika (Government securities) ili kurefusha kipindi cha kulipia madeni yake na hivyo kupunguza mzigo wa deni hilo katika bajeti ya serikali ya mwaka; na kuingiza dhamana na hatifungani (bonds) hizo katika soko la Hisa la Dar es Salaam ili kupanua biashara ya soko hilo.

Ujazi wa Fedha na Karadha

7. Sera za fedha na karadha zimelenga katika kupunguza na kutengamaza kasi ndogo ya upandaji bei na kufanikisha ukuaji wa uchumi. Katika mwaka ulioishia Desemba 2003, ujazi wa fedha kwa maana pana (M_2) uliongezeka kwa asilimia 14.1, ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 20.7 mwaka uliotangulia. Ujazi wa fedha katika kipindi hicho ulioongezeka kwa kiwango ambacho kilikuwa ndani ya lengo lililowekwa la asilimia 12.0 - 15.0. Kupungua kwa kasi ya ujazi wa fedha kulitokana na juhudi za Benki Kuu kufuatilia na kutengamaza ujazi wa fedha unaowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi. Mwenendo wa karadha kwa sekta binafsi katika kipindi hicho unaonyesha ongezeko kubwa la asilimia 43.2, na hivyo kuongeza kiasi cha mikopo inayotolewa na mabenki kwa sekta hiyo kufikia asilimia 98.4 ya mikopo yote. Mikopo iliyotolewa kwa serikali imepungua kwa kiasi kikubwa sana, kutoka asilimia 31.6 mwaka 2002 hadi asilimia 1.6 mwaka 2003. Kuongezeka kwa ushindani kati ya mabenki kumechangia katika kuongeza karadha kwa sekta binafsi.

Sekta ya Nje

8. Katika mwaka 2003, thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 26.6 kufikia dola za Marekani 1,142.4 milioni, ikilinganishwa na dola 902.5 milioni mwaka 2002. Mchango mkubwa katika mauzo hayo ulitokana na bidhaa zisizo asilia ambazo mauzo yake yaliongezeka kwa asilimia 32.0 kufikia dola 919.7 milioni, ikilinganishwa na dola 696.5 milioni mwaka 2002. Mauzo ya madini yameendelea kuchangia sehemu kubwa ya mauzo nje. Kwa mara ya kwanza baada ya zaidi ya miaka mitano mfululizo ya kupungua kwa mauzo nje ya bidhaa asilia, kulikuwa na ongezeko la asilia 8.1 kulikochangiwa na kuongezeka kwa bei na kiasi cha kahawa na pamba iliyouzwa mwaka 2003. Jedwali na. 4 linaonyesha mwenendo wa mauzo ya bidhaa nje. Thamani ya uagizaji kutoka nje iliongezeka kwa asilimia 30.5 kufikia dola 1,973.0 milioni, ikilinganishwa na dola 1,511.3 milioni mwaka 2002. Ongezeko hilo kubwa lilichangiwa na kuboreshwa kwa ukusanyaji taarifa za uingizaji wa bidhaa kutoka nje pamoja na ongezeko la uagizaji wa bidhaa za mitambo, malighafi za viwanda, na chakula. Jedwali Na. 5 linaonyesha mwenendo wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje, na Jedwali na. 6 linaonyesha mchanganuo wa mizania ya malipo nje.

Ukuaji wa Sekta Binafsi, Uwekezaji, na Marekebisho ya Mashirika ya Umma

9. Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuwezesha ukuaji na maendeleo ya sekta binafsi ikiwa pamoja na kuanzisha kitengo maalum (Better Regulation Unit, BRU) kinachoratibu utekelezaji wa mpango wa kuboresha/kuimarisha mazingira ya shughuli za sekta binafsi (Business Environment Strengthening in Tanzania, BEST), ikijumuisha biashara na uzalishaji mali mdogo na wa kati. Kitengo hicho pia kitaratibu shughuli ya utayarishaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta Binafsi (Private Sector Development Strategy) utakaobainisha na kuelekeza utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuendeleza sekta binafsi.

10. Kituo cha Uwekezaji (TIC) kimeendelea kuvutia wawekezaji nchini kwa kuongeza ufanisi katika huduma zake, ikiwa ni pamoja na kupunguza muda wa kukamilisha maombi, kuweka taarifa katika mtandao wa kompyuta kufuatilia shughuli za uwekezaji nchini (investor-tracking

system) na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji nchini kwa ujumla. Katika kipindi cha Januari – Desemba 2003, Kituo kiliidhinisha miradi 372 yenye thamani ya sh. 1,669.4 bilioni (sawa na dola za Marekani 1.6 bilioni), inayokadiriwa kutoa nafasi za ajira 198,458, ikilinganishwa na miradi 311 yenye thamani ya sh. 1,091.8 milioni iliyoidhinishwa mwaka 2002. Sekta ya Viwanda ilipata miradi mingi zaidi, ikiwa na miradi 127 (34%). Sekta nyingine zilizovutia wawekezaji wengi zaidi ni pamoja na sekta ya utalii iliyopata miradi 81 (22%), sekta ya ujenzi miradi 48 (13%), sekta ya usafirishaji miradi 28 (8%), sekta ya maliasili miradi 21 (6%) na sekta ya kilimo miradi 20 (5%). Katika mwaka 2003, thamani ya mitaji ya kigeni ya moja kwa moja (FDI) iliongezeka kwa asilimia 3.1 kufikia dola za Marekani 247.8, ikilinganishwa na dola 240.4 milioni mwaka 2002.

11. Hadi kufikia Desemba 2003, mali za umma 617 zilikuwa zimebinafsishwa, yakiwamo mashirika/kampuni 289. Katika mwaka 2003 peke yake, mali za umma 101 zilibinafsishwa, yakiwamo mashirika/kampuni 26. Mali zilizobinafsishwa mwaka 2003 ni pamoja na Kiwanda cha Karatasi (SPM), mahoteli ya TAHI (Manyara, Ngorongoro, Seronera na Lobo), Hoteli ya Kilimanjaro, na ukodishaji wa DAWASA. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika ubinafsishaji, bado kuna changamoto ya kuwapata wawekezaji wenye sifa na mitaji ya kutosha kuchukua mali zilizobaki, pamoja na mzigo wa madeni na wafanyakazi kwa baadhi ya mashirika yanayobinafsishwa. Aidha, baada ya ubinafsishaji wa mashirika na makampuni mengi ya umma, na kuingia katika uchumi wa soko huria, ili kulinda walaji na kutoa fursa sawa kwa wadau wote wa soko hilo, Serikali imeunda mamlaka za udhibiti na usimamizi kadhaa kwa madhumuni hayo. Mamlaka hizo ni EWURA (nishati na maji), SUMATRA (usafirishaji nchi kavu na majini), TCRA (mawasiliano), TGARA (ndege za serikali), na TCAA (ndege za kiraia).

Maendeleo ya Jamii na Mkakati wa Kupunguza Umaskini

12. Taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupunguza Umaskini ya mwaka 2002/03 imehitimisha awamu ya kwanza ya miaka mitatu ya utekelezaji wa mkakati huo. Taarifa hiyo inabainisha mafanikio na changamoto katika sekta mbalimbali na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa kipindi kijacho. Hata hivyo, katika matayarisho ya awamu ya

pili ya mkakati huo, mapitio ya kina yanafanywa na wadau mbalimbali ili kuhuisha mikakati na sera zote zinazoelekezwa katika kupambana na umaskini, ikiwa ni pamoja na kujizatiti zaidi katika utekelezaji wa mipango mbalimbali husika. Mapitio hayo yanatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2004. Matarajio ni kwamba awamu ya pili ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini itaandaliwa vizuri zaidi na kulenga katika maeneo yenye kuleta matokeo dhahiri. Taarifa za jumla katika utekelezaji wa mkakati huo, zinaonyesha kuboreshwa na kuimarika kwa huduma mbalimbali katika sekta za kipaumbele katika kupunguza umaskini kutokana na Serikali kuelekeza sehemu kubwa ya rasilimali za umma katika sekta hizo mwaka hadi mwaka. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na ongezeko la asilimia 50 katika uandikishaji watoto elimu ya msingi, walioongezeka kutoka milioni 4.4 mwaka 2000 hadi milioni 6.6 mwaka 2003. Kwa sehemu kubwa, ongezeko hilo limetokana na serikali kuondoa karo na michango mbalimbali katika shule za msingi pamoja na kupanua idadi ya madarasa. Chanjo kwa watoto wadogo (DPT) na surua imekuwa inaongezeka mwaka hadi mwaka hadi kufikia kiwango cha asilimmia 90. Takwimu thabiti za kupima maendeleo katika vigezo na viashirio mbalimbali vya maendeleo ya jamii zitapatikana kutokana na juhudi zinazofanywa na Serikali kuimarisha ukusanyaji, usambazaji na utunzaji wa takwimu za kiutawala, katika ngazi mbalimbali kutoka kijiji, kata, wilaya, mkoa hadi taifa.

MASUALA MUHIMU YA KISERA YALIYOJITOKEZA MWAKA 2003/04

13. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika mwaka 2003 ilipungua kutokana kwa sehemu kubwa, na kushuka kwa kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo iliyoathiriwa na ukame wa msimu wa 2002/03. Suala linalojitokeza ni jinsi ambavyo ukuaji wa uchumi wetu unaendelea kutegemea mwenendo wa sekta ya kilimo, ambao nao unategemea uwepo wa mvua ya kutosha. Changamoto iliyopo ni kuongeza juhudi katika kilimo cha umwagiliaji, katika mashamba madogo na makubwa, hususan, katika maeneo yasiyopata mvua za kutosha, lakini yana mito na mabonde yenye maji ya kutosha. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii, Serikali itaendelea kuboresha huduma za ughani na tafiti za kilimo, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo muhimu kwa wakulima, zikiwemo mbolea na mbegu bora, na

kuwezesha kupatikana kwa mikopo na dhamana kwa wakulima wakubwa na wadogo. Aidha, uboreshaji wa mtandao wa barabara kuu na za vijijini utachangia ongezeko katika uzalishaji. Ni muhimu pia kuimarisha uwezo wa kuhifadhi akiba ya chakula cha dharura ili kukidhi mahitaji ya chakula kunapotokea upungufu mkubwa utokanao na majanga yasiyotabirika.

14. Pamoja na kuwa na utaratibu mzuri wa kuandaa bajeti ya mwaka na ya upeo wa muda wa kati (MTEF), bado Serikali imekuwa na mahitaji ziada nje ya , hivyo kuwa vigumu kutekeleza bajeti nzima kama ilivyopangwa na kuidhinishwa na Bunge. Ukiacha dharura muhimu zisizotabirika, itabidi Serikali ijizatiti zaidi katika utaratibu wa kupanga na kutekeleza bajeti kama ilivyoidhinishwa. Utekelezaji wa miradi mingi ya maendeleo umeathirika kwa sababu mara nyingi mahitaji ya ziada nje ya bajeti hutumia fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo; hali ambayo imejenga dhana kuwa matumizi ya maendeleo (hususan fedha za ndani) hayana umuhimu kama matumizi ya kawaida. Aidha, nidhamu na ufanisi endelevu katika matumizi ya rasilimali itawezesha serikali kupanua upeo wa mikopo ya ndani kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hatuwezi kuendelea kutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za wafadhili kutekeleza miradi yote ya maendeleo.

15. Taarifa za Benki Kuu zinaonyesha kuwa mikopo inayotolewa na mabenki ya biashara kwa sekta binafsi imeongezeka sana (kiasilimia); lakini ukweli ni kwamba bado viwango vya mikopo hiyo ni vidogo, ikilinganishwa na uwezo wa mabenki hayo kukopesha. Sekta muhimu za uzalishaji, kama kilimo, hazipati mikopo ya kutosha. Baada ya kurekebisha Sheria ya Ardhi, kwa madhumuni ya kuipa thamani ya kuwezesha kutumika kama rehani katika mabenki, matumaini ni kwamba mikopo kwa sekta ya kilimo, na hasa kwa wakulima vijijini itaongezeka. Pia, marekebisho yanayoendelea katika sekta ya fedha yanatarajiwa kupunguza viwango vya riba kwa mikopo katika mabenki ya biashara na kuongeza riba kwa amana, ili kuhamasiha uwekaji wa akiba. Aidha, inabidi Benki Kuu ikamilishe utayarishaji wa taratibu na kanuni zinazohitajika kuongoza utoaji wa mikopo midogo midogo kwa wakulima na wajasiriamali wadogo na wa kati (regulatory and supervisory framework for microfinance institutions).

16. Mauzo ya bidhaa nje yanaonekana kuongezeka kwa kiasi kikubwa; hali ambayo imechangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu, samaki na bidhaa zake na bidhaa nyingine zisizo asilia. Hata hivyo, kuongezeka kwa mauzo ya dhahabu nje, bado hakujaiongezea Serikali mapato yake kwa kiasi cha kutosha, kwani makampuni makubwa yanayomiliki migodi ya dhahabu bado yana mikataba inayowapa nafuu ya kodi, ili walipie gharama za uwekezaji kutokana na mitaji waliyoipata nje ya nchi. Kwa hiyo, ili kuongeza manufaa yanayotokana na mauzo nje, kuna umuhimu katika kuongeza viwango vya ubora na wingi wa uzalishaji wa bidhaa nyingine, ikiwa ni pamoja na mpira (natural rubber) na za asilia kama kahawa na pamba ambazo bei ya soko la dunia imeanza kupanda. Aidha, kadri inavyowezekana, tulenge katika kuongeza thamani ya mauzo nje kwa kuyasindika hapa nchini. Katika mkakati wa kuongeza mauzo nje, ni muhimu kwa nchi yetu kujipanga vyema ili kukabiliana na changamoto na fursa zinazotokana na utandawazi na masoko ya kikanda kama EAC na SADC. Aidha, changamoto na fursa nyingine ni mipango ya AGOA (Marekani) na EBA (Jumuiya ya Ulaya).

17. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika urekebishaji wa mashirika ya umma na ubinafsishaji, na uendelezaji wa sekta binafsi, kumekuwa na changamoto kadhaa katika utekelezaji, kama malalamiko ya mafao kidogo, kukiuka mikataba ya mauzo na kuwa na sheria na taratibu zisizorandana. Hivyo, wakati tukijiandaa kubinafsisha mashirika makubwa yaliyobaki, ni vyema mafao ya wafanyakazi wanaoachishwa yakabainishwa mapema na jinsi ya kuyalipia. Vilevile, juhudi zaidi zinahitajika kuoanisha na kuendeleza sheria na taratibu zitakazowezesha kusukuma kwa kasi zaidi maendeleo ya sekta binafsi na ongezeko la mauzo nje.

MISINGI NA MALENGO YA SERA ZA UCHUMI JUMLA NA MAENDELEO YA JAMII KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI (2004/05 – 2006/07)

Misingi ya Matarajio

18. Maandalizi ya sera na malengo ya uchumi jumla na maendeleo ya jamii kwa kipindi cha muda wa kati (2004/05-2006/07) yamezingatia mambo yafuatayo:

- Ukame ulioathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo msimu wa 2002/03 hautarajiwi kuendelea, na hivyo uzalishaji wa sekta ya kilimo unatarajiwa kuongezeka na kuinua kasi ya ukuaji wa sekta hiyo kutokana na utekelezaji thabiti wa mipango ya kitaifa na kiwilaya ya kuendeleza kilimo. Kasi ya ukuaji wa sekta nyingine unatarajiwa kuongezeka k.m. viwanda, biashara (ikijumuisha utalii), uchukuzi na mawasiliano kufuatia hatua mbalimbali zilizochukuliwa na serikali, k.m. kuanzishwa kwa EPZ, ujenzi wa barabara, uwezeshaji katika uwekezaji na uzalishaji.
- Tutaendelea kutengemaza mazingiza ya uchumi jumla (macroeconomic stability), na hivyo kuwezesha ongezeko katika viwango vya uwekezaji nchini.
- Muda mfupi ujao, baada ya mavuno ya chakula kwa msimu wa 2003/04, kasi ya upandaji bei itaanza kuteremka.
- Hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kuongeza mapato, ikiwa ni pamoja na kuhuisha sheria husika, na misamaha ya deni la nje, kunatarijiwa kuongeza uwezo wa Serikali kutekeleza mipango yake muhimu, ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha matumizi ya maendeleo.
- Akiba ya fedha za nje inatarajiwa kuongezeka, kutokana na kuongeza mauzo nje na matarajio ya misaada zaidi.
- Mwenendo wa thamani ya shilingi ikilinganishwa na dola ya Marekani, itaendelea kudhibitiwa na mwenendo wa soko.

Malengo ya Sera za Uchumi Jumla na Maendeleo ya Jamii

19. Shabaha na malengo ya sera za jumla za uchumi yanaendelea kuwa ni kujenga uchumi ulio imara, unaokua na tengemavu. Katika jitihada za

kufanikisha hayo, malengo ya sera za uchumi jumla na maendeleo katika kipindi cha mwaka 2004/05 – 2006/07 yatakuwa yafuatayo:

- Pato la Taifa halisi linakadiriwa kukua kwa asilimia 6.3 mwaka 2004, asilimia 6.5 mwaka 2005, asilimia 6.9 mwaka 2006, na asilimia 7.4 mwaka 2007;
- Kasi ya upandaji bei itapungua hadi kufikia asilimia 4.0 ifikapo Juni 2005 na baadaye kupungua kwa kulingana na viwango vitakavyokuwepo katika nchi tunazofanya nazo biashara kubwa;
- Kuongeza mapato ya ndani yatakayofikia uwiano na Pato la Taifa, kwa bei za miaka husika, wa asilimia 15.1 mwaka 2004/05, hadi asilimia 16.2 ifikapo mwaka 2006/07;
- Kudhibiti ongezeko la ujazi wa fedha (kwa tafsiri pana, M_2) litakalowiana na malengo ya ukuaji wa uchumi, na kasi ya upandaji bei; na
- Kuwa na akiba ya fedha ya kigeni itakayoweza kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi sita.

HITIMISHO

Ni wajibu wa kila Wizara, Idara, Mkoa, Wilaya na Serikali za Mitaa kuzingatia mwelekeo wa misingi na malengo uliotolewa katika utayarishaji na utekelezaji wa mipango na bajeti katika miaka mitatu ijayo, katika kufanikisha juhudi za kutengemaza uchumi, kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi, na kuboresha maendeleo ya jamii.

Majedwali

Jedwali Na. 1: MUHTASARI WA VIASHIRIA MUHIMU VYA MWENENDO WA UCHUMI

	1996	1997	1998	1999	2000	2001	2002	2003
Ukuaji wa Pato Halisi - %	4.2	3.3	4.0	4.7	4.9	5.7	6.2	5.6
Kasi ya Upandaji bei (wastani kwa mwaka) - %	21.0	16.1	12.9	7.8	6.0	5.2	4.5	4.4
Thamani ya Shilingi (Tshs/USD) – wastani wa mwaka	580.0	612.1	664.7	744.8	808.4	876.4	966.6	1038.6
Thamani ya Shilinga (Tshs/USD) – mwisho wa mwaka	595.6	624.6	668.0	797.3	803.3	916.3	976.3	1063.6
Mauzo ya Bidhaa nje (mil. US$) - FOB	763.8	752.6	588.5	543.3	663.3	776.4	902.5	1142.4
Uagizaji wa Bidhaa toka nje (mil. USD) - FOB	1212.6	1148.0	1382.2	1415.4	1367.6	1560.3	1511.3	1973.0
Uwiano wa Mauzo ya Bidhaa Nje na Uagizaji - %	63.0	65.6	42.6	39.7	49.6	52.0	58.7	57.9
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamishomali	-265.1	-403.4	-905.4	-829.5	-498.6	-480.0	-251.1	-337.2
Uwianao wa Uwekezaji kwa Pato la Taifa ratio - %	16.5	14.7	16.0	15.4	17.6	17.0	18.9	18.5
Uwekezaji wa Moja kwa Moja (FDI) - mil. USD	148.5	157.8	172.2	516.7	463.4	327.2	240.4	247.8
Akiba ya Fedha za Kigeni Thamani ya miezi ya uagizaji)	2.4	3.8	3.0	4.1	5.6	6.3	8.3	8.9

	1996/97	1997/98	1998/99	1999/00	2000/01	2001/02	2002/03	2003/04[1]
Uwiano Mapato ya Ndani kwa Pato la Taifa (%)	13.5	12.6	12.5	11.3	12.2	12.1	12.8	13.4
Uwiano wa Matumizi yote kwa Pato la Taifa[2] (%)	17.3	17.4	17.6	18.3	20.6	19.1	23.4	24.9
Nakisi (Bila ya misaada) - % of GDPmp	-1.7	-2.3	-2.3	-5.8	-4.6	-5.6	-8.2	-11.2
Nakisi (Pamoja na misaada) - % of GDPmp	3.3	0.2	0.8	-1.6	-1.2	-1.1	-1.7	-4.0
Ukuaji wa Ujazi wa Fedha (M2) - %	11.6	11.0	11.1	15.0	12.5	12.3	13.0	14.2
Wastani wa Riba ya amana - %	11.0	10.0	7.9	7.1	4.2	3.5	3.1	3.9
Wastani wa Riba kwa mikopo - %	26.5	24.0	24.5	22.1	19.6	16.4	15. 7	13.8
Jumla ya mikopo (deni la nje) Iliyopokelewa (mil. USD)	6600.3	6435.8	6580.3	6538.3	6312.2	6559.7	6413.4	6730.8
Jumla ya madeni yote (mil. USD)[3]	7578.5	7384.6	7669.7	7624.8	7482.1	7464.0	7268.17	7890.7

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji, Benki Kuu ya Tanzania

[1] *Kama ilivyokuwa mwisho wa Desemba 2003*

[2] *Pamoja na malipo ya deni (mkopo + riba)*

[3] *Pamoja na riba kwa madeni yaliyotolewa*

Jedwali Na. 2: PATO LA TAIFA KISEKTA (Kwa bei za mwaka 1992)

Sh. milioni

	1997 Halisi	1998 Halisi	1999 Halisi	2000 Halisi	2001 Halisi	2002 Halisi	2003 Halisi.	2004 Makadirio	2005 Makadirio	2006 Makadirio	2007 Makadirio
Kilimo	726098	739942	770509	796513	840275	882090	917395	962947	1013327	1067891	1131831
Uchimbaji madini na mawe	24097	30700	33488	38144	43293	49787	56907	64176	71244	78031	85404
Bidhaa za Viwandani	117489	126887	131491	137809	144647	156219	169653	185237	202832	223615	249153
Umeme na maji	24514	25870	26874	28454	29297	30204	31669	32792	33756	35410	37837
Ujenzi	74361	65187	70866	76818	83494	92678	102872	111986	120435	131256	141027
Uuzaji wa Jumla, Rejareja na Mahoteli	229010	239830	254114	270567	288718	308928	329009	354034	381886	414726	452776
Mawasiliano na Uchukuzi	60079	79755	84403	89515	95154	101244	106357	113374	121376	131369	142770
Fedha, Bima, Mali na Huduma za kibiahara	149762	158089	164568	172291	177911	186485	194710	207068	220472	235714	253257
Uendeshaji Serikali na Huduma nyingine	115007	118114	122207	126567	130987	1136307	141880	148974	156423	164244	172948
To ushuru wa huduma za mabenki	-72327	-78548	-81229	-82359	-84418	-86781	-89819	-95520	-101703	-108734	-116827
Jumla ya Pato la Taifa	**1448089**	**1505826**	**1577291**	**1654319**	**1749358**	**1857158**	**1960633**	**2085068**	**2220048**	**2373522**	**2550176**
Mwaka wa Fedha	**1996/97**	**1997/98**	**1998/99**	**1999/00**	**2000/01**	**2001/02**	**2002/03**	**2003/04**	**2004/05**	**2004/06**	**2004/07**
Jumla ya Pato la Taifa	1424900	1476958	1541559	1615805	1701053	1803258	1908904	2022850	2152558	2296785	2461849

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji

Jedwali Na. 3: UKUAJI WA PATO LA TAIFA KISEKTA (Kwa bei za mwaka 1992)

	1997 Halisi	1998 Halisi	1999 Halisi	2000 Halisi	2001 Halisi	2002 Halisi	2003 Halisi	2004 akadirio	2005 Makadirio	2006 akadirio	2007 Makadirio
Kilimo	2.4 %	1.9 %	4.1 %	3.4 %	5.5 %	5.0 %	4.0 %	5.0 %	5.2 %	5.4 %	6.0 %
Uchimbaji madini na mawe	17.1 %	27.4 %	9.1 %	13.9 %	13.5 %	15.0 %	14.3 %	12.8 %	11.0 %	9.5 %	9.4 %
Bidhaa za Viwandani	5.0 %	8.0 %	3.6 %	4.8 %	5.0 %	8.0 %	8.6 %	9.2 %	9.5 %	10.2 %	11.4 %
Umeme na maji	2.2 %	5.5 %	3.9 %	5.9 %	3.0 %	3.1 %	4.9 %	3.5 %	2.9 %	4.9 %	6.9 %
Ujenzi	35.5 %	-12.3 %	8.7 %	8.4 %	8.7 %	11.0 %	11.0 %	8.9 %	7.5 %	9.0 %	7.4 %
Uuzaji wa Jumla, Rejareja na Mahoteli	5.0 %	4.7 %	6.0 %	6.5 %	6.7 %	7.0 %	6.5 %	7.6 %	7.9 %	8.6 %	9.2 %
Mawasiliano na Uchukuzi	-16.1 %	32.8 %	5.8 %	6.1 %	6.3 %	6.4 %	5.1 %	6.6 %	7.1 %	8.2 %	8.7 %
Fedha, Bima, Mali na Huduma za kibiahara	7.7 %	5.6 %	4.1 %	4.7 %	3.3 %	4.8 %	4.4 %	6.3 %	6.5 %	6.9 %	7.4 %
Uendeshaji Serikali na Huduma nyingine	3.2 %	2.7 %	3.5 %	3.6 %	3.5 %	4.1 %	4.1 %	5.0 %	5.0 %	5.0 %	5.3 %
Jumla ya Pato la Taifa	**3.3 %**	**4.0 %**	**4.7 %**	**4.9 %**	**5.7 %**	**6.2 %**	**5.6 %**	**6.3 %**	**6.5 %**	**6.9 %**	**7.4 %**
Mwaka wa Fedha	**1996/97**	**1997/98**	**1998/99**	**1999/00**	**2000/01**	**2001/02**	**2002/03**	**2003/04**	**2004/05**	**2005/06**	**2005/07**
Jumla ya Pato la Taifa	3.7%	3.7%	4.4%	4.8%	5.3%	6.0%	5.9%	6.0%	6.4%	6.7%	7.2%

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Rais – Mipango na Ubinafsishaji

Jedwali Na. 4: MAUZO YA BIDHAA ASILIA NA ZISIZO ASILIA NJE

US Dola milioni

	1999	2000	2001	2002	2003	Badiliko (%) 2002-2003
Bidhaa Asilia:						
Kahawa						
Thamani (US$ milioni)	**76.63**	**83.7**	**57.05**	**35.2**	**50.0**	**42.0%**
Kiasi ('000 Tani)	39.02	54.5	48.39	36.4	46.0	26.4%
Bei (US$ /Tani)	1963.80	1537.3	1179.06	968.4	1087.0	12.2%
Pamba						
Thamani (US$ milioni)	**28.46**	**38**	**33.7**	**28.6**	**46.6**	**62.9%**
Kiasi ('000 Tani)	26.31	36.8	36.82	33.3	46.9	40.8%
Bei (US$ /Tani)	1081.80	1031.3	915.26	859.4	992.8	15.5%
Katani						
Thamani (US$ milioni)	**7.26**	**5.6**	**6.68**	**6.6**	**6.6**	**0.0%**
Kiasi ('000 Tani)	15.47	13.3	13.86	12.7	12.8	0.01%
Bei (US$ /Tani)	469.17	420.8	482	516.4	517.8	0.0%
Chai						
Thamani (US$ milioni)	**24.65**	**32.7**	**29.03**	**29.6**	**24.8**	**-16.2%**
Kiasi ('000 Tani)	21.40	22.6	22.96	24.3	20.9	-14.0%
Bei (US$ /Tani)	1151.74	1450	1264.45	1217.8	1188.2	-2.4%
Tumbaku						
Thamani (US$ milioni)	**43.44**	**38.4**	**35.69**	**55.5**	**42.2**	**-24.0%**
Kiasi ('000 Tani)	21.35	19.2	18.72	24.3	20.3	-16.5%
Bei (US$ /Tani)	2034.44	1997.8	1906.17	2188.6	2076.1	-5.1%
Korosho						
Thamani (US$ milioni)	**100.89**	**84.4**	**56.58**	**46.6**	**42.2**	**-9.4%**
Kiasi ('000 Tani)	102.04	102.4	95.04	79.0	69.2	-12.4%
Bei (US$ /Tani)	988.78	824.5	595.38	589.7	609.5	3.4%
Karafuu						
Thamani (US$ milioni)	**19.86**	**10**	**12.32**	**4.0**	**10.3**	**157.5%**
Kiasi ('000 Tani)	6.21	2.9	2.45	1.0	5.6	460%
Bei (US$ /Tani)	3200.34	3443.6	5026.85	4164.4	1858.8	-55.4%
Jumla ndogo (US$ milioni)	**301.18**	**292.8**	**231.05**	**206.1**	**222.7**	**8.1%**
Bidhaa zisizo Asilia (US$ milioni):						
Madini:	**73.26**	**178.2**	**302.23**	**383.8**	**548.3**	**42.9%**
Dhahabu	34.77	112.7	254.07	341.1	499.0	46.3%
Almasi	20.05	42.2	27.08	22.0	28.6	30.0%
Madini mengineyo	18.44	23.3	21.08	20.7	20.7	0.0
Bidhaa za Viwanda:	**30.05**	**43.4**	**56.17**	**65.9**	**99.9**	**51.6%**
Nyuzi za Pamba	1.81	3.5	2.5	-	-	-
Kahawa iliyosindikwa	0.81	0.9	0.72	-	-	-
Tumbaku iliyosindikwa	0.82	0.1	0.13	-	-	-
Bidhaa za Katani (Nyuzi na Kamaba)	5.12	4.5	2.54	-	-	-
Bidhaa nyinginezo za Viwanda	21.49	34.4	50.28	-	-	-
Samaki na mazo ya Samaki	**56.75**	**76.3**	**96.77**	**116.8**	**136.2**	**16.6%**
Mauwa	**8.88**	**9.7**	**11.01**	**10.9**	**13.7**	**25.7%**
Bidhaa nyinginezo	**72.74**	**62.9**	**79.34**	**119.2**	**121.6**	**2.0%**
Jumla ndogo	**241.67**	**370.5**	**545.52**	**696.5**	**919.7**	**32.0%**
Jumla Kubwa (US$ milioni)	**542.85**	**663.3**	**776.37**	**902.5**	**1142.4**	**26.6%**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, Ofisisya Rais – Mipango na Ubinafsishaji

Kielelezo 1: MCHANGANUO (Kiasilimia) WA MAUZO NJE MWAKA 2003



Jedwali Na. 5: UAGIZAJI WA BIDHAA TOKA NJE

US Dola milioni

Aina ya Bidhaa	1999	2000	2001	2002	2003	Badiliko (%) 2002-2003
Bidhaa za Ukuzaji Rasilimali:	**770.1**	**638.7**	**739.7**	**721.1**	**852.4**	**18.2%**
Vifaa vya Usafirishaji	297.0	228.7	189.8	218.3	263.2	20.6%
Vifaa vya Ujenzi	132.0	128.9	144	134.7	168.3	24.99%
Mitambo	341.1	281.1	406	368.3	420.9	14.3%
Bidhaa za Kati:	**240.9**	**319.7**	**440.8**	**423.0**	**679.7**	**60.7%**
Mafuta	107.9	142.9	220.7	194.8	403.4	107.1%
o/w: Mafuta ghafi	77.9	131.9	0.0	0.0	0.0	0.0
Mafuta yaliyosafishwa	30.0	11.0	220.7	194.8	403.4	107.1%
Mbolea	13.5	16.8	15.5	20.1	28.5	41.8%
Malighafi ya Viwanda	119.5	160.0	204.6	208.0	247.7	19.1%
Bidhaa za Matumizi ya Kawaida:	**552.4**	**576.7**	**534.2**	**516.6**	**636.0**	**23.1%**
Chakula na bidhaa za vyakula	176.4	183.0	169.4	147.3	183.1	24.3%
Bidhaa nyinginezo	376.0	393.7	364.8	369.3	452.9	22.6%
Jumla Kubwa (C.I.F)	**1664.3**	**1535.1**	**1714.8**	**1660.8**	**2168.2**	**30.6%**
Jumla Kubwa (F.O.B)	**1497.9**	**1366.3**	**1560.5**	**1511.3**	**1973.0**	**30.5%**

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

Jedwali Na. 6: MIZANIA YA MALIPO NJE

US Dola milioni

	1996	1997	1998	1999	2000	2001	2002	2003
	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Halisi	Maka-dirio
Urari wa Biashara ya Bidhaa	**-448.8**	**-395.4**	**-793.7**	**-954.6**	**-703.1**	**-783.9**	**-608.7**	**-830.6**
Zilizouzwa nje (fob)	763.8	752.6	588.5	543.3	663.2	776.4	902.5	1142.4
Zilizonunuliwa toka nje (fob)	1212.6	1148.0	1382.2	1497.9	1366.3	1560.3	1511.3	1973.0
Urari wa Huduma	-278.8	-317.9	-463.1	-158	-86.8	-34.5	-46.7	-89.3
Mapato	537.1	482.4	538.8	622.0	643.8	679.3	665.8	685.2
Malipo	815.9	800.2	101.9	780.0	730.6	713.8	712.5	774.5
Urari wa Mapato ya Vitega Uchumi	-72.0	-121.8	-105.0	-99.3	-130.0	-85.2	-16.3	-43.7
Yaliyoingia	41.5	43.0	44.4	49.0	50.4	55.3	74.3	87.1
Yaliyotoka	113.5	164.8	149.4	148.3	180.4	140.5	90.6	130.8
Urari wa Uhamisho wa Kawaida	338.4	431.5	427.3	336.6	390.8	399.4	420.7	626.4
Iliyoingia	370.7	499.3	454.2	445.6	463.7	469.5	472.9	689.5
Serikalini	236.0	433.6	421.0	411.4	427.8	418.4	427.7	629.6
Misamaha ya HIPC [4]	0.0	0.0	0.0	0.0	40.6	71.3	68.8	68.2
Sekta zingine	134.7	65.7	33.2	34.2	35.9	51.1	45.2	69.9
Iliyotoka	32.3	67.7	26.9	109.0	72.9	70.0	52.3	63.0
Urari wa Biashara ya Bidhaa, Huduma na Uhamishomali	**-461.2**	**-403.6**	**-905.4**	**-829.5**	**-498.6**	**-480.0**	**-251.1**	**-337.2**
Urari wa Uhamisho wa Mitaji	191.0	270.9	252.4	270.6	330.4	365.2	354.1	677.7
Iliyoingia	191.0	270.9	252.4	270.6	330.4	365.2	354.1	677.7
Iliyotoka	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Urari katika uwekezaji	0.3	236.3	-166.1	613.3	572.5	98.2	295.9	129.3
Uwekezaji katika miradi	148.5	157.8	172.2	516.7	463.4	327.2	240.4	247.8
Uwekezaji katika hisa	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0	0.0
Uwekezaji aina nyingine	-148.2	78.5	-338.3	96.6	109.1	-229.0	55.5	-118.5
Makosa na Masahihisho	38.8	-303.6	313.3	-163.30	-439.5	34.1	-68.8	-67.0
Urari wa Malipo Yote	**-231.2**	**-199.8**	**-505.8**	**-109.0**	**-35.1**	**17.5**	**330.1**	**402.8**
Kujaza nakisi katika Urari wa Malipo	**231.2**	**199.8**	**505.8**	**109.0**	**35.1**	**17.5**	**-330.1**	**-402.8**
Akiba ya Fedha za Kigeni		-182.0	21.8	-175.5	-197.3	-186.6	-372.4	-508.8
Mikopo (IMF na mingineyo)		77.4	11.0	51.3	49.4	15.6	26.0	-2.9
Kusiko kwa Kawaida[5]		304.4	473.0	233.2	183.0	153.5	16.3	108.9

Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

[4] *Kutoka Mashirika ya Fedha ya Kimataifa (WB, IMF na ADB)*

[5] *Inajumuisha malimbikizo ya deni la nje (deni pamoja na riba) misamaha ya deni la nje na kuongeza muda wa malipo.*